

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 50 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** APRILI 2025

TSC YAANIKA MAFANIKIO YAKE MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN



MIKA
MINNE 4

YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



1. Walimu 227,383 wamepandishwa vyeo
2. Walimu 52,106 wamethibitishwa kazini
3. Walimu 37,473 walijajiwa na kusajiliwa
4. Ujenzi wa jengo la TSC Makao Makuu unaogharimu bilioni 6.45 wafikia 51%
5. Mfumo wa TSCMIS wajengwa na kuanza kutumika
6. Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wapya wanaojiriwa kwenye Utumishi wa Umma na Mwongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma imeandaliwa
7. Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma umeandaliwa

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

KONGOLE RAIS SAMIA KWA KULETA MAGEUZI MAKUBWA KATIKA SEKTA YA ELIMU

kiwa miaka minne (4) imekamilika tangu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani tarehe 19 Machi, 2021 tumeshuhudia mapinduzi makubwa katika maendeleo ya Sekta ya Elimu jambo linalofanya Taifa letu kuongeza kasi ya maendeleo.

Mabadiliko katika Sekta ya Elimu yamegusa nyanja mbalimbali ikiwemo walimu kutatuliwa changamoto zilizokuwa zinawakabili ikiwa ni pamoja na kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu, kubadilishiwa vyeo, kuendelea kulipwa fedha za malimbikizo mishara na likizo, ujenzi wa nyumba za walimu, ukarabati na ujenzi wa madarasa na shule pamoja na ujenzi wa maabara.

Vilevile, Serikali ya Rais Samia itaendelea kukumbukwa kwa uamuzi wake wa kuandaa Sera na Mtaala mpya wa elimu jambo ambalo linaongeza fursa za wanafunzi katika soko la

ajira pale wanapohitimu elimu zao.

Tunaamini kuwa Rais Samia bado ana malengo makubwa katika kuendelea kuboresha elimu ya Tanzania, na hii imethibitishwa kwa namna ambavyo anaendelea kutafuta fedha ndani na nje ya nchi huku fedha nyingi zikielekezwa katika Sekta ya Elimu.

Nimuhimu kila mmoja kuendelea kumuunga mkono Rais Samia ili tuendele kushuhudia mabadiliko zaidi ya maendeleo katika Sekta hii muhimu. Hongera sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa uchapakazi wako uliotukuka. Walimu wana imani kubwa na wewe na wataendelea kukuunga mkono ili yale yote uliyopanga yafanyike katika Sekta ya Elimu yaweze kutimia kwa ajili ya Ustawi wa Watanzania Wote.

Kazi iendele.....

KATUNI

BODI YA UHARIRI

UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU

AJIRA MPYA ZA WALIMU

SERA NA MTAALA MPYA

MIUNDOMBINU



Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge

Mectildis F. Kapinga

Lameck S. Mbeya

Zachary A. Dida

Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz

Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, S.L.P 353, DODOMA.



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

TSC YAANIKA MAFANIKIO YAKE MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akibadilishana marwazo na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) mara baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mjini Dodoma tarehe 15 Juni, 2024.

// Mimi nawapenda sana walimu... nawapenda kwa sababu wanasaidia kuelimisha umma wetu...umma wa Watanzania, walimu wanafanya kazi nzito...Walimu chapeni kazi mama yupo pamoja nanyi" **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

Rais Samia katika kudhihirisha kauli yake katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake amefanya juhudi kubwa za kutatua kero mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili walimu zikiwemo za upandishwaji madaraja, mapunjo ya mishahara, madai ya nauli za likizo, posho za uhamisho na matibabu.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (Teachers' Service Commission - TSC) Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tangu aliingie madarakani tarehe 19 Machi, 2021 ameendelea kutatua kero mbalimbali za walimu na kuiwezesha Tume kama msimamizi wa walimu wa Shule za Msingi na

Sekondari Tanzania bara.

"Tunamshukuru sana Rais Samia kwa kuendelea kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake. Imani aliyonayo Mhe. Rais wetu kwetu sisi watumishi wa Tume kwa kushirikiana na Wajumbe wa Tume ni kuhakikisha tunasimamia utumishi wa walimu kikamilifu ili walimu wetu watimize wajibu wao ipasavyo lakini pia wapate haki zao kwa ujibu wa sheria," alisema.

Katibu huyo wa Tume alisema kuwa tangu Rais Samia alipoingia madarakani tarehe 19 Machi, 2021 hadi Machi 2025, jumla ya walimu 227,383 Walipandishwa vyeo, kati yao walimu wa Shule za Msingi ni 145,699 na Sekondari ni 81,684.

Aliongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne(4) imethibitisha jumla ya walimu 52,106 ambapo kati yao walimu wa Shule za Msingi ni 21,405 na Sekondari ni 16,068.

Aidha, alisema kuwa katika kipindi hicho jumla ya walimu 37,473 walisajiliwa, kati yao walimu wa Shule za Msingi ni 21,405 na Sekondari ni 16,006.

Mwl. Paulina alisema kuwa katika

kipindi cha miaka minne (4), jumla ya walimu 37,473 walijajiwa ambapo Walimu wa Shule za Msingi ni 21,405 na Sekondari ni 16,068 ikijumuisha na Mafundi Sanifu Maabara 62 na kuongeza kuwa katika kipindi cha miaka minne (4) jumla ya walimu 24,881 walibadilishiwa vyeo baada ya kujiendeleza.

Aliongeza kuwa Rais Samia kupitia miradi ya Shule Bora imewezesha TSC kuchapisha nakala 7,893 za vitabu vya Sheria ya TSC kwa lugha rahisi kwa shule zote zilizopo katika mikoa 9 ya mradi wa Shule Bora.

Mwl. Paulina alisema kuwa Uongozi wa Awamu ya Sita imesaidia kugharimia mafunzo kuhusu mfumo wa TSC MIS kwa Maafisa wa Tume na Maafisa TEHAMA (ICTO) katika Halmashauri 79 nchini.

Alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita kupitia miradi ya GPE imeiwezesha Tume ya Utumishi wa Walimu kuandaa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wapya wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma na Mwongozo wa Mafunzo na Usimamizi wa Masuala ya nidhamu na rufaa kwa walimu katika Utumishi wa Umma Mafunzo juu ya Miongozo hiyo yanaendelea kutolewa.

UJENZI WA OFISI ZA TUME MAKAO MAKUU

Mwl. Paulina alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia imetenga Shilingi 6,499,982,353.03 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Tume ya Utumishi wa Walimu kwenye eneo la uwekezaji Njedengwa jijini Dodoma.

Baada ya Serikali kutenga kiasi hicho cha fedha, TSC iliingia Mkataba na SUMA JKT Kanda ya Kati kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Tume ya Utumishi wa Walimu.

Alisema kuwa hadi kufikia Februari, 2025 Tume ya Utumishi wa Walimu imepokea na kutumia kiasi cha shilingi 658,347,581.00 ambapo mradi huu umefikia asilimia 51 ya utekelezaji.

Mwl. Paulina alisema kuwa

INAENDELEA UK. 4

TSC YAANIKA MAFANIKIO YAKE MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

INATOKA UK. 3

shughuli zilizofanyika ni kujenga nguzo za sakafu ya tatu ambapo mradi huo unatarajia kukamilika Mei, 2025 kwa mujibu wa mpango kazi na mkataba mpya alioongezewa Mkandarasi.

MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC MANAGEMENT INFORMATION SYSTEM – TSCMIS)

Serikali ya Awamu ya Sita imeiwezesha Tume kujenga Mfumo wa Kielektroniki wa Tume unaojulikana kama “Teachers Service Commission Management Information System” (TSCMIS).

Mwl. Paulina alisema kuwa lengo ni kuboresha na kurahisisha utendaji kazi wa shughuli za kila siku katika kuwahudumia walimu na Wadau mbalimbali.

Alisema kuwa Mfumo huu umeandaliwa kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za kiutendaji kufuatia matumizi ya Mfumo wa sasa usio wa kielektroniki (Manual System) zikiwemo kutokuwa na taarifa sahihi za walimu (unreliable data), kutumia gharama kubwa na muda mrefu kushughulikia na kufuatilia masuala mbalimbali ya walimu na kushindwa kushughulikia masuala ya Nidhamu,



Washiriki wa kikao kazi cha wataalamu wakiandaa rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa walimu katika Utumishi wa Umma tarehe 23 Novemba, 2024 mjini Morogoro.

Rufaa na Malalamiko ya walimu kwa ufanisi.

Mwl. Paulina alisema kuwa Mfumo huo umesaidia kuboresha utekelezaji wa majukumu katika kuwahudumia walimu kwa wakati na kwa ufanisi, umerahisha mchakato wa kushughulikia mashauri ya Nidhamu na Rufaa za walimu kuanzia ngazi ya Shule, Wilaya hadi Makao Makuu na umerahisisha zoezi la kutoa namba za usajili kwa walimu (TSC Number).

Faida nyingine za mfumo huo

ni kutoa Mkataba na barua za ajira pamoja na barua nyingine kadri zitakavyohitajika.

Mfumo umesaidia Walimu kupata huduma wakiwa katika vituo vya kazi na kuwaondolea usumbufu wa kufuata huduma katika Ofisi za Tume ngazi ya wilaya na umesaidia upatikanaji wa taarifa kwa wakati na kwa usahihi.

Aliongeza kuwa Tume kupitia bajeti ya maendeleo ya mwaka 2022/23 imefanikiwa kusimika miundombinu ya mtandao wa intaneti katika Ofisi za Wilaya 26 katika Mikoa mitano (5) ya Mwanza, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Shinyanga na wilaya mbili (2) za Mkoa wa Morogoro ambazo ni Mvomero na Morogoro.

Katibu huyo wa Tume alisema kuwa wamefanikiwa kufungamanisha (integration) Mfumo wa TSCMIS na Mifumo mitatu (3), e-Watumishi, School Information System (SIS) na Treasury Pensioners Payment System (TPPS) lengo likiwa ni kubadilisha taarifa muhimu za walimu na kuboresha utendaji kazi, kuwa na taarifa sahihi katika kushughulikia masuala ya Ajira, Nidhamu, Rufaa na Mafao kwa walimu ambapo taarifa hizo pia zikichakatwa zitatumika katika kutoa maamuzi mbalimbali.



Mtaalamu wa Mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) kutoka TSC Makao Makuu, Pastory Munyaki akiwasilisha mada kuhusu namna ya kutumia mfumo huo kwa walimu wa shule ya Sekondari Dodoma Novemba 2, 2023.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)



MIAKA
MINNE 4

YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



1. Walimu 227,383 wamepandishwa vyeo
2. Walimu 52,106 wamethibitishwa kazini
3. Walimu 37,473 walijajiwa na kusajiliwa
4. Ujenzi wa jengo la TSC Makao Makuu unaogharimu bilioni 6.45 wafikia 51%
5. Mfumo wa TSCMIS wajengwa na kuanza kutumika
6. Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wapya wanaojajiwa kwenye Utumishi wa Umma na Mwongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma imeandaliwa
7. Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma umeandaliwa

Hongera! na Kazi lendelee!



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

NKM TAMISEMI AWATAKA MAKATIBU WASAIDIZI TSC KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUZUIA UKIUKAJI WA MAADILI YA KAZI

Na Mwandishi Wetu – Tabora.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Bw. Atupele Mwambene amewataka Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoa elimu kwa walimu ili kuzuia kuingia katika ukiukaji maadili ya kazi ya ualimu jambo linalosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kupewa adhabu mbalimbali ikiwemo kufukuzwa kazi.

Ametoa kauli hiyo tarehe 4 Machi, 2025 wakati akifungua Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu

Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora.

Alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ya siku tatu ni kuwajengea uwezo Makatibu Wasaidizi wa Tume Ngazi ya Wilaya na Maafisa wa Tume ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aliongeza kuwa TSC ipo kwa ajili ya kusaidia walimu kupata uelewa juu ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayohusu utumishi wao hivyo, inapaswa kutoa elimu mara kwa mara badala ya kusubiri matatizo yatokee kwa walimu ndio waanze kutoa elimu.

“Tume ni chombo Mahususi kwa ajili ya kushughulika na masuala ya utumishi wa walimu, hivyo mtambue na kutekeleza kikamifu eneo la kutoa elimu kwa walimu, tuwe walezi bora kwa walimu hatupaswi kufurahia kufukuza kazi walimu,” alisisitiza.

Bw. Mwambene alisema kuwa Miongozo iliyoandaliwa ina lengo la kuweka kinga zaidi ya kuzuia ukiukwaji wa maadili ya Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma miongoni kwa walimu ili isaidie kuongeza tija katika kutoa huduma bora kwa wanafunzi.

Awali Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa TSC kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais TAMISEMI inatekeleza Programu ya miaka minne (2023/24 hadi 2026/27) ya uboreshaji wa Kada ya Ualimu (Teachers’ Support Programme -TSP).

Alisema kuwa Tume inatekeleza afua zinazosaidia kutoa motisha na uwajibikaji kwa walimu lengo likiwa ni kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa ajili ya kuleta mageuzi katika sekta ya elimu nchini.

Mwl. Paulina alisema kuwa katika utekelezaji wa mradi Tume ya Utumishi wa Walimu ina jukumu la kuandaa na kusambaza Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wanaoajiwa upya katika Utumishi



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Bw. Atupele Mwambene akitoa hotuba ya ufunguzi wa Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora tarehe 4 Machi, 2025.

wa Umma huku akiongeza kuwa linalotekelezwa ni kuendesha mafunzo kwa Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu kuhusu uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na Rufaa kwa walimu.

Aidha, Mwl. Paulina alitaja mada zitakazofundishwa kwa Makatibu Wasaidizi hao ni pamoja na utaratibu wa kusimamia masuala ya nidhamu kwa walimu, mchakato wa kuendesha mashauri ya nidhamu na rufaa na kushughulikia masuala ya nidhamu yasiyo ya jinai.

Mafunzo hayo ya siku tatu yameshirikisha Makatibu Wasaidizi wapatao 139 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora tarehe 4 Machi, 2025.

NKM TAMISEMI AWATAKA MAKATIBU WASAIDIZI TSC KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUZUIA UKIUKAJI WA MAADILI YA KAZI



Mwakilishi wa Katibu Tazwala wa Mkoa wa Tabora, Bw. Elihuruma Nyela akitoa salam wakati wa ufunguzi wa Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora tarehe 4 Machi, 2025.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Tabora, Bw. Simon Mengo akitoa neno la shukrani mara baada ya ufunguzi wa Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora tarehe 4 Machi, 2025.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Bw. Atupele Mwambene (Katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora.

NKM TAMISEMI AWATAKA MAKATIBU WASAIDIZI TSC KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUZUIA UKIUKAJI WA MAADILI YA KAZI



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Bw. Atupele Mwambene (katikati) akiingia ukumbini kwa ajili ya kufungua Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora tarehe 4 Machi, 2025. Pichani, upande wa kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.



Washiriki wa Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya wakiwa kwenye hafla ya ufunguzi wa mafunzo hayo tarehe 4 Machi, 2025. yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora.

Kutoka Bungeni jijini Dodoma kwenye Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kinachoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Justine Nyamoga, wajumbe, viongozi pamoja na watendaji wa OR – TAMISEMI wakipitia randama ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2025/26 tarehe 19.03.2025.



Kutoka Bungeni jijini Dodoma kwenye Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kinachoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Justine Nyamoga, wajumbe, viongozi pamoja na watendaji wa OR – TAMISEMI wakipitia randama ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2025/26 tarehe 19.03.2025.



Kutoka Bungeni jijini Dodoma kwenye Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kinachoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Justine Nyamoga, wajumbe, viongozi pamoja na watendaji wa OR – TAMISEMI wakipitia randama ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2025/26 tarehe 19.03.2025.



TSC KONGWA YAPONGEZA UONGOZI WA RAIS SAMIA KWA KUONDA KERO ZA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Kongwa.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kongwa imempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za kutatua kero mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili walimu katika Wilaya hiyo.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kongwa, Bw. Edward Chamwela wakati wa mahojiano wa Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu.

Alisema kuwa uongozi wa Awamu ya Sita, umesaidia kutatua kero ya madaraja kwa Walimu, na kupunguza malalamiko kwa kiasi kikubwa ambapo jumla ya walimu 1,027 wamepandishwa madaraja ikiwa Shule za Msingi ni 714 na Sekondari ni 313

Alisema kuwa hatua alizochukua Rais Samia kwa upande wa Kongwa zimesaidia walimu kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

"Katika awamu ya sita ya uongozi



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kongwa, Bw. Edward Chamwela akiendelea kutekeleza majukumu ofisini kwake.

wa Mhe. Rais Mama Samia Suluhu Hassan, Ofisi inajivunia kitendo cha kuruhusu upandishaji wa vyeo kwa walimu ambapo walimu wamepata unafuu wa maisha na sasa wanafanya kazi kwa bidii kwa lengo la kuboresha elimu," alisema.

Aliongeza kuwa uongozi wa Awamu ya Sita umejitahidi

kuhakikisha madeni ya walimu yanayotokana na likizo na uhamisho katika Wilaya ya Kongwa yanalipwa kwa wakati.

Aidha, Bw. Chamwela alisema kuwa Tume inaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuiwezesha fedha kwa ajili ya utoaji mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi mbalimbali wanaosimamia walimu wilayani humo.

Alisema kuwa kupitia uwezesaji huo wa Serikali waliweza kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Wilaya ambayo yamesaidia kutoa elimu ya uelewa wa pamoja kwa TSC na kazi zake na wajumbe wameelimishwa juu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na kazi ya ualimu.

Bw. Chamwela alisema kuwa mafunzo kwa Wakuu wa shule yamesaidia kuwajengea uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa walimu na hivyo kutekeleza majuku yao kwa weledi.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kongwa inahudumia jumla ya shule 159 zikiwemo 121 za msingi na 38 za Sekondari huku idadi ya walimu ikiwa ni 1,785 kwa shule za msingi ni 1,250 kwa upande wa sekondari ni 535.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kongwa Bw. Edward Chamwela (wa kwanza kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimimu wa Wilaya hiyo.

MAKATIBU WASAIDIZI TSC TEKELEZENI MAJUKUMU YENU KWA WELEDI - SACP MAHUMI



Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimali Watu Serikalini Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, SACP Ibrahim Mahumi akitoa hutuba ya kufunga mafunzo ya Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu yaliyofanyika kwa siku tatu katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tawi la Tabora hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu-TSC-Tabora

Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wametakiwa kutumia mafunzo waliyopata kuhusu Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye utumishi wa umma na Mafunzo Elekezi ya Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu ili kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimali Watu Serikalini Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora SACP Ibrahim Mahumi, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Bw. Juma Mkomi wakati wa kufunga mafunzo ya siku tatu ya Makatibu Wasaidizi hao yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tawi la Tabora.

"Ni imani yangu kwamba, mmepata uelewa mkubwa kuhusu uzingatiji wa Sheria Kanuni na Taratibu zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yenu... hivyo, ninawataka muendeleo kutekeleza jukumu lenu la msingi ambalo ni usimamizi wa

Utumishi wa Walimu lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa tunakuwa na walimu wenye kujituma na wanaozingatia maadili ya kazi yao katika kuwalea Watoto wetu," alisema.

Aidha, Mkurugenzi huyo aliwataka Makatibu Wasaidizi wasaidie kuelimisha jamii kuwa ajira za ualimu hivi sasa zinatolewa kwa ushindani ili kuhakikisha wanapatikana walimu wenye sifa nzuri ikiwa ni pamoja na maadili mazuri kazini.

Alisema kuwa kabla ya utaratibu huo wapo walimu walikuwa wakichukuliwa na kufanya vitendo ambavyo ni kinyume na utumishi wa umma na utumishi wa Walimu.

Vilevile, SACP Mahumi, aliwahiza Makatibu Wasaidizi hao na Watumishi wa umma kuendelea na ujazaji wa utekelezaji wa majukumu yao katika Mfumo wa upimaji wa utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma ujulikanao kama PEPMIS.

"Kuna watu walisema kuwa mfumo huu utakufa nawaambia upo na uteandelea kuwepo, hivyo kwa Watumishi wote wa umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa kila wiki wanajaza majukumu yao... kwa mtumishi ambaye atashindwa kufikisha walau alama 75 yuko hatarini

katika utumishi wake," alisema.

Aliongeza kuwa madhara ya wale ambao watahindwa kutekeleza majukumu yao na kujaza utekelezaji watakuwa katika hatari kufungiwa mishahara na kuchukulia hatua za kinidhamu.

Awali, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikishirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, inatekeleza Programu ya miaka minne (2023/24 - 2026/27) ya Uboreshaji wa Kada ya Ualimu (Teacher Support Programme - TSP).

Alisema lengo la program hiyo ni kuboresha mazingira ya ufundishaji kwa walimu na ujifunzaji kwa wanafunzi ili kuinua kiwango cha elimu inayotolewa nchini kwa kuzingatia mabadiliko makubwa yanayotokea katika elimu ikiwemo Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2024 toleo la 2023 na Mitaala iliyoboreshwa.

Alisema kuwa katika utekelezaji wa programu ya GPE TSP, Tume ya Utumishi wa Walimu ina jukumu la kuandaa na kusambaza Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma na Kufanya Mafunzo kwa Watumishi wa Tume kuhusu Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu.

Mwl. Paulina alisema kuwa mafunzo hayo yalikusisha Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma na Mafunzo ya Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu yakihusisha mada mbalimbali zilizomo kwenye Miongozo hiyo Miwili iliyoandaliwa na Tume.

Alitaja mada zilizowasilishwa katika mafunzo hayo kuwa ni; utaratibu wa kusimamia masuala ya nidhamu kwa walimu, taratibu na hatua za kushughulikia makosa mepesi na mazito kwa walimu, mchakato wa kuendesha mashauri ya kinidhamu kwa makosa mazito na mepesi kwa walimu, ushughulikiaji wa masuala ya nidhamu yenye jinai na utaratibu wa rufaa katika utumishi wa walimu.

Mafunzo hayo ya siku tatu yaliwahusisha Kaimu Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu kutoka Wilaya zote za Tanzania Bara.

MAKATIBU WASAIDIZI TSC TEKELEZENI MAJUKUMU YENU KWA WELEDI - SACP MAHUMI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa kufunga mafunzo ya Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu yaliyofanyika kwa siku tatu katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tarwi la Tabora hivi karibuni.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyela, Bw. Julius Mwambogela akitoa neno la shukrani wakati wa kufunga mafunzo ya Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu yaliyofanyika kwa siku tatu katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tarwi la Tabora hivi karibuni.



Washiriki wa mafunzo ya Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiimba wimbo wa Taifa wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku tatu katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tarwi la Tabora hivi karibuni.

MAKATIBU WASAIDIZI TSC TEKELEZENI MAJUKUMU YENU KWA WELEDI - SACP MAHUMI



Picha ya pamoja kati ya Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimali Watu Serikalini Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, SACP Ibrahim Mahumi (katikati) na baadhi washiriki wa mafunzo ya Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa kufunga mafunzo hayo mjini Tabora hivi karibuni.



Washiriki wa mafunzo ya Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku tatu katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tarwi la Tabora hivi karibuni.



MAKATIBU WASAIDIZI TSC TEKELEZENI MAJUKUMU YENU KWA WELEDI - SACP MAHUMI



Washiriki wa mafunzo ya Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku tatu katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tarwi la Tabora hivi karibuni.



KUTUNUKIWA CHETI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akipokea cheti cha ushiriki Mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora hivi karibuni.



Washiriki mbalimbali wa mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya wakipokea vyeti wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora hivi karibuni.

KUTUNUKIWA CHETI



Washiriki mbalimbali wa mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya wakipokea vyeti wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora hivi karibuni.

KUTUNUKIWA CHETI



Washiriki mbalimbali wa mafunzo ya Usimamizi wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kwa Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya wakipokea vyeti wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika katika Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Tabora hivi karibuni.

TSC YAPONGEZA JUHUDI ZA RAIS SAMIA KWA KUWEZESHA UJENZI WA MFUMO WA TSCMIS



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama akifungua mafunzo ya kujengeana uwezo Katibu Wasaidizi na maafisa wa TSC ngazi ya Wilaya kuhusu ufanyaji kazi wa mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) tarehe 12 Machi, 2025 jijini Arusha.

Na Mwandishi Wetu -TSC

Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) imepongeza juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Tume hiyo kujenga Mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha na kuboresha utendaji kazi wa TSC katika kutoa huduma kwa walimu.

Pongezi hizo zimetolewa tarehe 12 Machi, 2025 na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama jijini Arusha wakati akifungua mafunzo ya kujengeana uwezo kuhusu ufanyaji kazi wa mfumo wa TSCMIS kwa Katibu Wasaidizi wa TSC Ngazi za Wilaya.

"Namshukuru sana Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri na kubwa anayofanya kwa Tume na taifa kwa ujumla kuhakikisha kuwa walimu wanahudumiwa ipasavyo,"alisema.

Mwl. Paulina aliongeza, "hii ni pamoja na kuwezesha mafunzo haya muhimu chini ya ufadhili wa wadau wetu wa maendeleo Shule Bora ili kuwaongezea watumishi wa Tume ujuzi na weledi zaidi katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ya kutoa huduma kwa na kwa ufanisi haraka kwa Walimu."

Alisema kuwa mfumo huo utasaidia kupunguza matumizi ya karatasi kwa Tume kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya.

Aidha, Mwl. Paulina alisema kuwa Mfumo huo unajumuisha moduli sita (6) ambazo ni usimamizi wa mashauri ya nidhamu, usimamizi na rufaa, usajili wa Walimu, usimamizi wa Pension, mirathi na mikataba ya walimu wa kabla ya Julai, 2004 (wanaolipwa na Hazina), malalamiko na Dawati la msaada; na usimamizi na Uratibu na Wageni.

Alisema kuwa faida za Mfumo wa TSCMIS kwa Tume na wadau ni pamoja na kuboresha utekelezaji wa majukumu katika kuwahudumia Walimu kwa wakati na ufanisi, utarahisisha mchakato wa kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za Walimu kuanza ngazi ya Shule na Ofisi za Wilaya hadi Makao Makuu.

Mwl. Paulina alisema kuwa faida nyingine utasaidia kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa hatua za Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kuanzia ngazi ya Shule hadi Makao Makuu, utapunguza makosa, gharama, muda na kuongeza ufanisi wa kushughulikia mashauri ya nidhamu na Rufaa za Walimu, Mfumo utarahisisha mchakato wa kuwasilisha vielelezo (viambatisho) mbalimbali

vinavyohusu masuala ya Mashauri ya Nidhamu, Rufaa Malalamiko, Mafao na Mirathi.

Alisema kuwa pia Mfumo utarahisisha zoezi la kutoa Namba za Usajili za Walimu (TSC Number), utakuwa na uwezo wa kutoa taarifa (notification) zilizopokelewa na kuwasilishwa kuhusu masuala ya Mashauri ya Nidhamu, Rufaa, malalamiko, mafao na mirathi, utakuwa na uwezo wa kutoa mrejesho (feedback) kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa, mfumo utapunguza matumizi ya karatasi na kuboresha utunzaji na upatikanaji wa taarifa, utarahisisha upatikanaji wa tarifa mbalimbali kwa wakati, utarahisisha mawasiliano na utendaji kazi katika Ofisi za Tume kuanzia ngazi ya Wilaya, Makao Makuu na Wadau mbalimbali na utasimamia na kutunza rekodi za wageni.

Alisema kuwa mafunzo hayo ni mwendelezo wa mafunzo ambayo yametolewa katika awamu mbili yaliyojumuisha watumishi wa Makao Makuu na Ofisi za wilaya kutoka katika mikoa 12.

Mwl. Paulina alisema kuwa katika awamu hii mafunzo yanafanyika Kanda ya Arusha inayojumuisha Kaimu Katibu Wasaidizi na Afisa mmoja mmoja kutoka katika Ofisi za wilaya kwenye Mkoa wa Arusha, Manyara na Kilimanjaro pamoja na Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wawili (2) kutoka Arusha CC & DC.

Alisema kuwa lengo la kujumuisha Maafisa TEHAMA ni kuhakikisha wanapata uelewa wa mafunzo ili kuweza kutoa msaada wa kitaalam wa haraka kwa Maafisa wa Tume pindi itakapohitajika kufanya hivyo.

Mwl. Paulina alisema kuwa mafunzo hayo yataendelea kutolewa kwa Maafisa TEHAMA ili kuhakikisha Maafisa wote katika Halmashauri wanapata uelewa wa matumizi ya Mfumo huu.

TSC YAPONGEZA JUHUDI ZA RAIS SAMIA KWA KUWEZESHA UJENZI WA MFUMO WA TSCMIS



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama akifungua mafunzo ya kujengeana uwezo Katibu Wasaidizi na maafisa wa TSC ngazi ya Wilaya kuhusu ufanyaji kazi wa mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) tarehe 12 Machi, 2025 jijini Arusha.



Baadhi ya Kaimu Makatibu Wasaidizi kutoka Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara wakiwa katika mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu ufanyaji kazi wa mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) tarehe 12 Machi, 2025 jijini Arusha.



Baadhi ya Kaimu Makatibu Wasaidizi kutoka Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara wakiwa katika mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu ufanyaji kazi wa mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) tarehe 12 Machi, 2025 jijini Arusha.

TSC MPWAPWA YAELEZA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpwapwa Bw. Mawazo Tulyanje Sephania akiendelea kutekeleza majukumu ofisini kwake wilayani Mpwapwa.

Na Mwandishi Wetu – Mpwapwa.

Tume ya utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mpwapwa imefafanua namna Serikali inavyowajibika kushughulikia haki za walimu ikiwepo masuala ya kupandishwa vyeo na kubadilishwa muundo kwa wakati.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mpwapwa, Bw. Mawazo Sephania wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha TSC.

Alisema kuwa uongozi wa Awamu ya Sita, umefanikiwa kutatua kero ya madaraja kwa Walimu, na kupunguza malalamiko kwa kiasi kikubwa ambapo jumla ya walimu 769 wamepandishwa madaraja katika mwaka wa fedha 2023/2024 ikiwa Shule za Msingi ni 493 na Sekondari ni 276.

Alieleza kuwa hatua alizochukua Rais Samia katika kulinda maslahi ya

walimu, kwa upande wa Mpwapwa zimesaidia walimu kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

“Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2023/24 tulipandisha vyeo walimu 769 hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu,” alisema.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema Rais Samia ameendelea kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu katika Wilaya ya Mpwapwa kwa kuruhusu walimu kuajiriwa ambapo kwa mwaka 2022/23 jumla ya walimu 170 wa walisajiliwa ikiwa wa Shule ya Msingi ni 108 na shule za Sekondari 62 na kuongeza kuwa walimu 167 walithibishwa kazini ambapo Msingi 108 na Sekondari 59.

Alifafanua kuwa dhamana ya kupandisha vyeo walimu ipo mikononi mwa Kamati ya TSC Wilaya

kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 huku akibainisha kuwa kwa upande wa Mpwapwa Kamati hiyo ilihakikisha kuwa kila mwalimu aliyekuwa na sifa ya kupanda cheo kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa alipata haki hiyo.

Aidha, Bw. Sephania alisema kuwa Tume inaishukuru Serikali ya Awamuya Sita kwa kuiwezesha fedha kwa ajili ya utoaji mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi mbalimbali wanaosimamia walimu wilayani humo.

Alisema kuwa kupitia uwezesaji huo wa Serikali waliweza kutoa mafunzo kwa wajumbe wa kamati za Wilaya ambayo yamesaidia kutoa elimu ya uelewa wa pamoja kwa TSC na kazi zake na wajumbe wameelimishwa juu Sheria, Kanuni, Taratibu za utumishi wa walimu.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Sephania alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpwapwa imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Aliendelea kusema pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

Bw. Sephania alifafanua kuwa katika kipindi cha mwaka 2023/2024, TSC wilaya ya Mpwapwa ilipokea na kushughulikia jumla ya mashauri 12 ikiwa Shule za Msingi 7 na Sekondari 5.

Alisema kuwa walimu 04 walifukuzwa kazi, walimu 05 hawakupatikana na hatia, Walimu 03 walisamehewa.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpwapwa inahudumia jumla ya shule 172 zikiwemo 135 za msingi na 37 za Sekondari huku idadi ya walimu ikiwa ni 1,549 kwa shule za msingi ni 1,075 kwa upande wa sekondari ni 474.

TSC MPWAPWA YAELEZA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpwapwa Bw. Marwazo Tulyanje Sephania (wa kwanza kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Tume wa Wilaya hiyo.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mpwapwa Bw. Marwazo Tulyanje Sephania (wa kwanza kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Tume na walimu waliotembelea ofisi hiyo kwa lengo la kupata huduma.

MAAFISA 229 WA TSC WAJENGEWA UWEZO WA MATUMIZI YA MFUMO WA TSCMIS

Na Mwandishi Wetu – Arusha.

Jumla ya Maafisa 229 wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Maafisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika baadhi ya Halmashauri nchini wamejengewa uwezo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) wakati wa utoaji huduma kwa walimu.

Mafunzo hayo yalianza tarehe 12 na kumalizika tarehe 14 Februari, 2025 katika Kanda nne ambazo ni Mbeya iliyokuwa na Washiriki 85, Arusha washiriki 38, Mwanza washiriki 70 na washiriki 36.

Lengo la Mafunzo hayo ya siku tatu ni kuwasaidia watumishi wa Tume na wadau mbalimbali katika kusimamia na kushughulikia masuala ya Utumishi wa Walimu kwa kutumia mfumo huo.

Katika mafunzo hayo, washiriki walifundishwa moduli (vipengele) sita ambazo ni usimamizi wa mashauri ya nidhamu (Disciplinary Management), usimamizi wa rufaa (Appeal Management) – usajili wa walimu (teachers registration), usimamizi wa pension, mirathi na mikataba wa walimu wa kabla Julai, 2004 (Gratuity Computation & Management), malalamiko na dawati la msaada (Query & Helpdesk Management) na usimamizi na uratibu na wageni (visitors management).

Akifunga mafunzo hayo tarehe 14 Februari, 2025, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama aliwataka washiriki wanaporudi kwenye vituo vyao vya kazi wakatoe huduma kwa walimu kwa wakati, ufanisi na weledi.

Aliwataka kutumia mafunzo hayo kurahisisha utoaji wa huduma kwa usahihi na kupunguza matumizi ya makaratasi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa ni vema wakaendeleza ushirikiano na mawasiliano ili waweze kukwamuana wanapotekeleza majukumu yao kupitia Mfumo huo.

"Naamini wawezeshaji wetu watatufungulia kundi sogozi kwa



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akifunga mafunzo ya siku tatu ya kujengeana uwezo kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) Watumishi wa Tume wanapotekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yalifungwa tarehe 14 Februari, 2025 jijini Arusha.

ajili ya kurahisisha mawasiliano na kuendelea kuimarishana kutumia mfumo huu kwa vitendo, pamoja na kusaidiana kutatua changamoto tutakazokutana nazo katika kutumia mfumo huu," alisema.

Mwl. Paulina aliongeza, "Natarajia mtakuwa Champion wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa mujibu wa Sheria Sura ya 448 kwa kutumia mfumo wetu wa Kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS)."

Aidha, aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa

utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa mfumo huo ambao narahisisha utoaji wa huduma kwa walimu.

Halikadhalika, Mwl. Paulina aliishukuru SHULE BORA kwa kuwezesha mafunzo hayo kufanyika huku Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mkinga, Mwl. Juma Selemeni akiushukuru uongozi wa Tume kwa kuwapa mafunzo hayo na kuahidi kutumia mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) kutoa huduma nzuri kwa wadau wao wakiwemo walimu.

MAAFISA 229 WA TSC WAJENGEWA UWEZO WA MATUMIZI YA MFUMO WA TSCMIS



Baadhi ya Makatibu Wasaidizi kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara wakifuatilia hotuba ya ufungaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu ufanyaji kazi wa mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) jijini Arusha.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Tume kutoka Mkoa wa Arusha mara baada ya hotuba yake ya kufunga mafunzo ya siku tatu ya kujengeana uwezo kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) wakati wa Watumishi wa Tume wanapotekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yamefungwa tarehe 14 Februari, 2025 jijini Arusha.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Tume kutoka Mkoa wa Manyara mara baada ya hotuba yake ya kufunga mafunzo ya siku tatu ya kujengeana uwezo kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) wakati wa Watumishi wa Tume wanapotekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yamefungwa tarehe 14 Februari, 2025 jijini Arusha.

MAAFISA 229 WA TSC WAJENGEWA UWEZO WA MATUMIZI YA MFUMO WA TSCMIS



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Tume kutoka Mkoa wa Kilimanjaro mara baada ya hotuba yake ya kufunga mafunzo ya siku tatu ya kujengeana uwezo kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) wakati wa Watumishi wa Tume wanapotekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yamefungwa tarehe 14 Februari, 2025 jijini Arusha.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wawezeshaji wa Mafunzo mara baada ya hotuba yake ya kufunga mafunzo ya siku tatu ya kujengeana uwezo kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) wakati wa Watumishi wa Tume wanapotekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yamefungwa tarehe 14 Februari, 2025 jijini Arusha.

Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mkinga, Mwl. Juma Selemani akitoa neno la shukurani kwa Mgeni rasmi mara baada ya kufunga mafunzo ya siku tatu ya kujengeana uwezo kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) wakati wa Watumishi wa Tume wanapotekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yamefungwa tarehe 14 Februari, 2025 jijini Arusha.

KATIBU WA TUME YA UTUMISHI AWAONGOZA MAMIA KUMUAGA MTUMISHI WA TUME, 'DON' URASSA

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama tarehe 18 Machi 2025 ameongoza mamia ya viongozi, Watumishi wa TSC, Watumishi wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, viongozi wa dini na wananchi mbalimbali katika kuaga mwili wa Mtumishi wa Tume, Bw. Raymond Rogasian Urassa maarufu kama 'Don Urassa' aliyefariki tarehe 13 Machi, 2025 katika Hospitali ya Benjamiin Mkapa jijini Dodoma.

Akizungumza na Mwandishi wa Habari hizi, alisema kuwa atamkumbuka Bw. Urassa kwa uchapaji kazi pamoja na ushirikiano wake na watumishi wote wa Tume.

Mwl. Paulina alisema kuwa msiba huo umewagusa wengi hasa watumishi wa TSC kwani siku chache kabla ya kifo chake, marehemu Raymond Urassa alikuwa anaendelea kutekeleza majukumu yake ya kiofisi kama kawaida.

"Kifo cha Urassa kimeniumiza sana...kwani kabla sijasafiri kikazi alifika Ofisini kwangu akiwa na afya nzuri...niliposikia amefariki nishituka sana...lakini yote ni mipango ya Mungu," alisema.

Akiwasilisha salamu za Mwajiri wakati wa Misa ya kumuaga Marehemu Raymond, Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Zachary Dida alisema kuwa marehemu ameacha pengo kubwa katika familia ya watumishi wa Tume.

Alisema kuwa wakati wa utumishi wake katika Ofisi ya Tume wa Utumishi wa Walimu alitekeleza majukumu yake kwa ushirikiano na Watumishi wote na alikuwa mkarimu kwa kila mtumishi bila kujali umri wala cheo.

Bw. Dida alisema kuwa kwa upande wa Watumishi wa Tume waliobakia amewaachia funzo kubwa la kuwa na upendo katika katika kutoa huduma kwa wadau mbalimbali.

"Urassa alikuwa rafiki wa kila



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama akitoa heshima za mwisho tarehe 18 Machi, 2025 wakati wa kuaga mwili wa mtumishi wa TSC, marehemu, Raymond Rogasian Urassa maarufu kama 'Don Urassa' aliyefariki tarehe 13 Machi, 2025 katika Hospitali ya Benjamiin Mkapa jijini Dodoma.

mtu pale ofisini, Urassa alikuwa mcheshi lakini Urassa alikuwa anachangamana na watu wa rika zote...kwa hiyo naweza kusema Urassa alikuwa rafiki wa watu wote pale ofisini alipokuwa akifanyia kazi...tunajua Urassa tutaendelea kumkumbuka kwa yale mema aliyoyafanya wakati wa uhai wake," alisema Dida.

Akizungumza katika Misa iliyofanyika nyumbani kwa marehemu, Padri Leadry Kimario alisema kuwa Bw. Raymond katika uhai wake alijaliwa kipaji cha upendo ambapo alipenda familia yake na watu wanaomzunguka.

Aliwaasa wanafamilia na jamii waliomjua marehemu Raymond kuendeleza mambo mazuri aliyoyatekeza wakati wa uhai wake.

Akiongoza misa katika Parokia ya Watakatifu Wote iliyopo Nzuguni jijini Dodoma, Fr. Perfect Leiya alisema kuwa Bw. Raymond alikuwa mtu aliyejitolea sana katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya kanisa ikiwa ni pamoja na kuwajali viongozi wa kiroho.

Baada ya misa hiyo, mwili wa marehemu Urassa ulisindikizwa na mamia ya waombolezaaji hadi kwenye makaburi ya Nzuguni ambapo mazishi yalifanyika.

KATIBU WA TUME YA UTUMISHI AWAONGOZA MAMIA KUMUAGA MTUMISHI WA TUME, 'DON' URASSA



Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Zachary Dida akitoa salamu za Mwakiri wakati wa adhimisho la Misa ya kumuaga aliyekuzwa mtumishi wa Tume, marehemu Raymond Rogasian Urassa maarufu kama 'Don Urassa' aliyefariki tarehe 13 Machi, 2025 katika Hospitali ya Benjamiin Mkapu jijini Dodoma.



Padri Perfect Leiya akihubiri kwenye adhimisho la Misa Kanisani katika Parokia ya Watakatifu Wote kumuaga Dereva wa Tume Bw. Raymond Rogasian Urassa maarufu kama 'Don' Urassa kanisani leo tarehe 18 Machi, 2025 jijini Dodoma.



Padri Leadry Kimario kutoka Chuo cha Mwenge Jimbo la Moshi akiongoza mazishi ya aliyekuwa mtumishi wa TSC, marehemu Raymond Rogasian Urassa katika makaburi ya Nzuguni jijini Dodoma tarehe 18 Machi, 2025.



Baadhi ya waombolezaji wakiwa nyumbani kwa marehemu Raymond Urassa wakati wa adhimisho la Misa ya kumuaga iliyofanyika tarehe 18 Machi, 2025 jijini Dodoma.



KATIBU WA TUME YA UTUMISHI AWAONGOZA MAMIA KUMUAGA MTUMISHI WA TUME, 'DON' URASSA



Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Zachary Dida akiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa mtumishi wa Tume, marehemu Raymond Rogasian Urassa maarufu kama 'Don Urassa' katika makaburi ya Nzuguni jijini.



Mke wa marehemu Raymond Rogasian Urassa (kushoto) akiweka shada la maua kwenye kaburi la mume wake tarehe 18 Machi, 2025.



Waombolezaji mbalimbali wakiweka maua kwenye kaburi la aliyekuwa mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, marehemu Raymond Rogasian Urassa wakati wa mazishi yake yaliyofanyika katiaka makaburi ya Nzunguni jijini tarehe 18 Machi, 2025.



Waombolezaji mbalimbali wakiwa katika mazishi ya aliyekuwa mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, marehemu Raymond Rogasian Urassa wakati wa mazishi yake yaliyofanyika katiaka makaburi ya Nzunguni jijini tarehe 18 Machi, 2025

Baadhi ya Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika picha ya pamoja nyumbani kwa aliyekuwa mtumishi wa TSC, marehemu Raymond Urassa wakati wa msiba wa mtumishi huyo tarehe 18 Machi, 2025.



KATIBU WA TUME YA UTUMISHI AWAONGOZA MAMIA KUMUAGA MTUMISHI WA TUME, 'DON' URASSA





MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu